# Habakuki

1 Neno la unabii alilopokea nabii Habakuki.

### *Lalamiko la Habakuki*

2 Ee Mwenyezi Mungu, hata lini nitakuomba msaada,
lakini wewe husikilizi?
Au kukulilia, “Udhalimu!”
lakini hutaki kuokoa?
3 Kwa nini unanifanya nitazame dhuluma?
Kwa nini unavumilia makosa?
Uharibifu na udhalimu viko mbele yangu;
kuna mabishano na mapambano kwa wingi.
4 Kwa hiyo sheria imepotoshwa,
nayo haki haipo kabisa.
Waovu wanawazunguka wenye haki,
kwa hiyo haki imepotoshwa.

### *Jibu la Mwenyezi Mungu*

5 “Yatazame mataifa,
uangalie na ushangae kabisa.
Kwa sababu katika siku zako nitafanya kitu
ambacho hungeamini,
hata kama ungeambiwa.
6 Tazama! Nitawainua Wakaldayo,
watu wakatili na wenye haraka,
ambao hupita dunia yote
ili kuteka makazi yasiyo yao.
7 Ni watu wanoogopwa na wanaotisha;
wenyewe ndio sheria yao,
na huinua heshima yao wenyewe.

8 Farasi wao ni wepesi kuliko chui,
na wakali kuliko mbwa-mwitu wakati wa machweo.
Askari wapanda farasi wao huenda mbio;
waendesha farasi wao wanatoka mbali.
Wanaruka kasi kama tai
ili kurarua mawindo;
9 wote wanakuja tayari kutenda udhalimu.
Makundi yao wanasonga mbele
kama upepo wa jangwani,
na kukusanya wafungwa
kama mchanga.
10 Wanawabeza wafalme,
na kuwadhihaki watawala.
Wanaicheka miji yote yenye ngome;
wanalundika udongo na kuiteka hiyo miji.
11 Kisha wanapita kasi kama upepo na kusonga mbele:
watu wenye hatia, ambao nguvu zao ndio mungu wao."

### *Lalamiko la pili la Habakuki*

12 Ee Mwenyezi Mungu, je, wewe sio wa tangu milele?
Mungu wangu, Uliye Mtakatifu wangu, hatutakufa.
Ee Mwenyezi Mungu, umewachagua wao ili watekeleze hukumu;
Ee Mwamba, umewaamuru watuadhibu.
13 Macho yako ni safi mno hata yasiweze kuutazama uovu,
wala huwezi kuvumilia makosa.
Kwa nini basi unawavumilia wadanganyifu?
Kwa nini unakuwa kimya wakati waovu
wanawameza wale wenye haki

kuliko wao wenyewe?
14 Umewafanya watu kama samaki baharini,
kama viumbe wa bahari wasio na mtawala.
15 Adui mwovu anawavuta wote kwa ndoana,
anawakamata katika wavu wake,
anawakusanya katika juya lake;
kwa hiyo anashangilia na anafurahi.
16 Kwa hiyo anatoa sadaka kwa wavu wake,
na kuchoma uvumba kwa juya lake,
kwa kuwa kwa wavu wake anaishi kwa starehe,
na anafurahia chakula kizuri.
17 Je, aendelee kuwatoa walio katika wavu wake,
akiangamiza mataifa bila huruma?

# 2

1 Nitasimama katika zamu yangu,
na kujiweka juu ya maboma;
nitatazama nione atakaloniambia,
na jibu nitakalotoa kuhusu lalamiko hili.

### *Jibu la Mwenyezi Mungu*

2 Kisha Mwenyezi Mungu akajibu:
“Andika ufunuo huu,
na ukaufanye wazi juu ya vibao,
ili mpiga mbiu akimbie nao.
3 Kwa kuwa ufunuo huu unasubiri wakati uliokubalika;
unazungumzia mambo ya mwisho,
na kamwe hautakosea.
Iwapo utakawia, wewe usubiri;
kwa hakika utakuja na hautachelewa.

4 “Tazama, amejaa majivuno;

anavyovitamani si vya unyofu:
lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake:
5 hakika mvinyo humsaliti;
ni mwenye kiburi na hana amani.
Kwa sababu ni mlafi kama Kuzimu*,
na kama kifo kamwe hatosheki;
anajikusanyia mataifa yote
na kuchukua watu wote mateka.
6 “Je, watu wote hawatamsuta kwa dhihaka na
kumbeza, wakisema,
“ ‘Ole wake yeye akusanyaye bidhaa zilizoibwa
na kujifanyia utajiri kwa kutoza kwa nguvu!
Ataendelea hivi kwa muda gani?’
7 Je, wadai wako hawatainuka ghafula?
Je, hawataamka na kukufanya utetemeke?
Kisha utakuwa mhanga kwao.
8 Kwa kuwa umeteka nyara mataifa mengi,
watu waliobaki watakuteka nyara wewe.
Kwa kuwa umemwaga damu ya watu;
umeharibu nchi na miji, na watu wote wanaoishi humo.

9 “Ole wake yeye ajengaye milki yake kwa mapato ya udhalimu,
awekaye kiota chake juu,
ili kukimbia makucha ya uharibifu!
10 Umepanga njama ya maangamizi ya watu wengi,
ukiaibisha nyumba yako mwenyewe,
na kupotewa na maisha yako.
11 Mawe ya kuta yatapiga kelele,

* **2:5** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

na mihimili ya kazi ya mbao itarudisha
mwangwi wake.

12 “Ole wake yeye ajengaye mji kwa kumwaga
damu na kuusimamisha mji kwa uhalifu!
13 Je, Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni hakuonesha
kwamba kazi ya wanadamu ni mafuta tu
kwa ajili ya moto,
na kwamba mataifa
yanajichosha bure?
14 Kwa kuwa dunia itajazwa na maarifa ya
utukufu wa Mwenyezi Mungu,
kama maji yaifunikavyo bahari.

15 “Ole wake yeye awapaye majirani zake kileo,
akikimimina kutoka kwa kiriba cha mvinyo
hadi wamelewa,
ili apate kutazama miili yao iliyo uchi.
16 Utajazwa na aibu badala ya utukufu.
Sasa ni zamu yako! Kunywa na ujifunue!
Kikombe kutoka mkono wa kuume wa Mwenyezi
Mungu kinakujia,
na aibu itafunika utukufu wako.
17 Ukatili ulioifanyia Lebanoni utakufunika,
na uharibifu uliowafanyia wanyama
utakutisha.
Kwa sababu umemwaga damu ya mtu;
umeharibu nchi na miji na kila mmoja aliye
ndani yake.

18 “Sanamu ina thamani gani,
kwani mwanadamu ndiye alichonga?

Ama kinyago kinachofundisha uongo?
Kwa kuwa yeye aliyekitengeneza
hutegemea kazi ya mikono yake mwenyewe;
hutengeneza sanamu zisizoweza kuzungumza.
19 Ole wake yeye auambiaye mti, ‘Uwe hai!’
Ama asemaye na jiwe lisilo na uhai, ‘Amka!’
Je, linaweza kuongoza?
Limefunikwa kwa dhahabu na fedha;
hakuna pumzi ndani yake.
20 Lakini Mwenyezi Mungu yuko katika Hekalu lake takatifu;
dunia yote na inyamaze mbele yake.”

# 3

*Maombi ya Habakuki*

1 Sala ya nabii Habakuki iliyoimbwa kwa shigionothi*.
2 Mwenyezi Mungu, nimezisikia sifa zako;
nami naogopa kwa matendo yako, Ee Mwenyezi Mungu.
Fufua kazi yako katika siku hizi zetu,
tangaza habari yako wakati huu wetu;
katika ghadhabu kumbuka rehema.

3 Mungu alitoka Temani,
yeye Aliye Mtakatifu kutoka Mlima Parani.
Utukufu wake ulifunika mbingu,
na sifa zake zikaifunika dunia.
4 Mng’ao wake ulikuwa kama jua linapochomoza;

* **3:1** Ni kifaa cha uimbaji chenye nyuzi; pia maombi kutumia kifaa hiki.

miali ilimulika kutoka mkononi mwake,
ambako nguvu zake zilifichwa.
5 Tauni ilimtangulia;
maradhi ya kuambukiza yalifuata nyayo zake.
6 Alisimama, akaitikisa dunia;
alitazama, na kuyafanya mataifa yatetemeke.
Milima ya zamani iligeuka mavumbi
na vilima vilivyozeeka vikaanguka.
Njia zake ni za milele.
7 Niliona watu wa Kushani katika dhiki,
na makazi ya Midiani katika maumivu makali.

8 Ee Mwenyezi Mungu, uliikasirikia mito?
Je, ghadhabu yako ilikuwa dhidi ya vijito?
Je, ulighadhibikia bahari
ulipoendesha farasi wako
na magari yako ya vita ili ushinde?
9 Uliufunua upinde wako
na kuitisha mishale mingi.
Uliigawa dunia kwa mito;
10 milima ilikuona ikatetemeka.
Mafuriko ya maji yakapita huko;
vilindi vilinguruma
na kuinua mawimbi yake juu.

11 Jua na mwezi vilisimama kimya mbinguni
katika mng'ao wa mishale yako inayoruka,
na katika mng'ao wa mkuki wako umeremetao.
12 Kwa ghadhabu ulipitia kwenye dunia,
na katika hasira ulikanyaga mataifa.

13 Ulikuja kuwaokoa watu wako,
kumwokoa uliyempaka mafuta.
Ulimponda kiongozi wa nchi ya uovu,
ukamvua toka kichwani hadi wayo.
14 Kwa mkuki wake mwenyewe ulitoboa kichwa chake
wakati mashujaa wake walifurika nje kwa kishindo kututawanya,
wakifurahi kama walio karibu kutafuna
wale wanyonge waliokuwa mafichoni.
15 Ulikanyaga bahari kwa farasi wako,
ukisukasuka maji makuu.

16 Nilisikia na moyo wangu ukagonga kwa nguvu,
midomo yangu ikatetemeka kwa hofu niliposikia sauti;
uchakavu ukanyemelea mifupa yangu,
na miguu yangu ikatetemeka.
Hata hivyo nitasubiri kwa uvumilivu siku ya maafa
kuyajilia mataifa yaliyotuvamia.
17 Ingawa mtini hauchanui maua
na hakuna zabibu juu ya mizabibu,
ingawaje mzeituni hauzai,
na hata mashamba hayatoi chakula,
iwapo hakuna kondoo katika banda,
wala ng'ombe katika zizi,
18 hata hivyo nitashangilia katika Mwenyezi Mungu,
nitamfurahia Mungu Mwokozi wangu.

19 Bwana Mungu Mwenyezi ni nguvu yangu;
huifanya miguu yangu kama miguu ya ayala,

huniwezesha kupita juu ya vilima.
Kwa kiongozi wa uimbaji. Kwa vinanda vyangu vya nyuzi.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu
## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible." Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d